


DCB COMMERCIAL BANK

# MKUTANO MKUU WA 23 WA MWAKA NA TAARIFA YA BENKI KWA MWAKA 2024





# “TUNASTAWI PAMOJA NAWE”

Kaulimbiu ya mwaka huu, “TUNASTAWI PAMOJA NAWE”, inaakisi dhamira ya benki ya DCB ya kuchochea ustawi wa uchumi kwa kushirikiana na wateja katika safari yao ya maendeleo. Tunaamini kwamba mafanikio ya kweli yanawezekana kwa kufanya kazi kwa pamoja. Kupitia huduma zetu na mwendo wa kidijitali, tunalenga kuwa chachu ya mabadiliko chanya katika maisha ya kila mteja.




VIFUPISHO
**06**

23.2 TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 23 WA MWAKA
**08**

23.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 22 WA MWAKA
**09-12**

23.4 KUPOKEA NA KURIDHIA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA MKUTANAO MKUU WA 22 WA MWAKA
**13**

23.5 KUPOKEA TAARIFA YA WAKURUGENZI WA BODI
**14-26**

23.6 KUPOKEA NA KURIDHIA MAPENDEKEZO YA MABADILIKO YA VIFUNGU VYA KATIBA YA BENKI
**26-27**

23.7 KURIDHIA UTEUZI WA WAJUMBE WA BODI
**28**

23.8 KUTEUA MKAGUZI HURU WA HESABU KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 31 DISEMBA 2025
**28**

23.9 KUPOKEA NA KURIDHIA PENDEKEZO LA MALIPO YA ADA KWA WAJUMBE WA BODI
**28**

23.10 KUPANGA TAREHE YA MKUTANO MKUU WA 24 WA MWAKA
**28**

KIAMBATANISHO NA 1
**29-32**

KIAMBATANISHO NA 2
**33-34**

# TAARIFA ZA KAMPUNI

**OFISI ILIYOSAJILIWA**

Jengo la DCB House
Kitalu Na. 182 - R
Magomeni Mwembechai
S.L.P 19798
Dar es Salaam

**KATIBU WA KAMPUNI**

Ms Regina Mduma
Jengo la DCB House
Kitalu Na. 182 – R
Magomeni Mwembechai
S.L.P 19798
Dar es Salaam

**WAKAGUZI**

KPMG
The Luminary
Plot No.574, Haile Selassie Road
Msasani Peninsula Area
S.L.P 1160
Dar es Salaam

**WANASHERIA**

Excellent Attorneys
$5^{th}$ Floor Citi Plaza Building
Jamhuri Street
Dar es Salaam

Breakthrough Attorneys
66 BTA House, Plot No 331/10
Msasani Road, Oyster Bay
Opposite United Nations,
Umoja House
PS.L.P 72838
Dar es Salaam

Lawfront Advocates
S.L.P 31312
Mikocheni A, Garden Road
Dar es Salaam

Apex Attorneys Advocates
$1^{st}$ Floor, Scouts Building
Malik Road, Upanga
S.L.P 34674
Dar es Salaam



# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AGM | Mkutano Mkuu wa Mwaka |
| ATM | Mashine ya kutoa na kuweka fedha |
| ALCO | Kamati ya Mali na Dhima |
| BOT | Benki Kuu ya Tanzania |
| CIR | Uwiano wa mapato na matumizi |
| CMSA | Mamlaka ya masoko ya mitaji na dhamana |
| DCB | Benki ya biashara ya DCB |
| DSE | Soko la Hisa la Dar-es-Salaam |
| EAD | Kadirio la hasara ya mikopo isiyolipika ya benki |
| ECL | Matarajio ya baadaye ya hasara ya mikopo |
| EPS | Mapato yatokanayo na hisa |
| IASB | Bodi ya Viwango ya Uhasibu ya Kimataifa |
| IESBA | Bodi ya Viwango ya Maadili ya Kimataifa ya Wahasibu |
| IFRS | Viwango vya Kimataifa vya Taarifa za Fedha |
| LC | Barua za mikopo |
| LDR | Mkopo kwa uwiano wa amana |
| LGD | Hasara itokanayo na mikopo usiyolipika |
| NPL | Mikopo chechefu |
| POCI | Mali zinazotarajiwa kusababisha hasara |
| ROUA | Haki ya Matumizi ya Mali |
| SGL | Ukopaji wa vikundi |
| SICR | Ongezeko kubwa la hatari ya mikopo |
| SME | Wafanyabiashara wadogo wadogo na kati |
| SMR | Kiwango cha chini cha amana cha kisheria |
| SPPI | Malipo ya Kianzio na Riba |
| SPV | Kampuni ya makusudio maalum |
| TMRC | Taasisi ya Mikopo ya Nyumba ya Tanzania |
| TSH | Shilingi ya Kitanzania |
| USD | Dola ya Marekani |

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 23 WA MWAKA



## 23.2 TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 23 WA MWAKA

Taarifa inatolewa kwamba, Mkutano Mkuu wa 23 wa mwaka wa Benki ya DCB, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 19 Julai, 2025 kwa njia ya mtandao (Zoom Conference), kuanzia saa nne kamili asubuhi.

### AGENDA

1. Kufungua mkutano mkuu wa mwaka
2. Kuridhia agenda ya Mkutano Mkuu wa 23 wa mwaka
3. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 22 wa mwaka uliofanyika tarehe 14 Septemba, 2024
4. Kupokea na kuridhia utekelezaji wa yatokanayo na Mkutano Mkuu wa 22 wa mwaka
5. Kupokea na kuridhia
    - 5.1 Taarifa ya wakurugenzi ya mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2024
    - 5.2 Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2024
    - 5.3 Taarifa ya mkaguzi huru ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2024
6. Kupokea na kuridhia Mabadiliko ya Vifungu vya Katiba ya Kampuni
7. Kuridhia uteuzi wa wajumbe wa Bodi
8. Kuteua mkaguzi huru wa hesabu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2025
9. Kupokea na kuridhia pendekezo la malipo ya ada kwa wajumbe wa bodi
10. Kupanga tarehe ya Mkutano Mkuu wa ishirini na nne
11. Mengineyo
12. Kufunga mkutano

### MAELEZO

1. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria Mkutano Mkuu wanatakiwa wawe na CDS namba ambazo zinapatikana kwenye risiti ya uwekezaji wa hisa (depository receipt) au taarifa ya akaunti (CSDR account statement).

2. Wanahisa ambao hawataweza kuhudhuria Mkutano Mkuu wanaruhusiwa kuchagua wawakilishi watakaohudhuria na kupiga kura kwa niaba yao kwa kuzingatia sheria na Katiba ya Kampuni. Fomu ya uwakilishi (Proxy Form) lazima ijazwe na kuwasilishwa kwenye ofisi ya Katibu wa Benki iliyopo Makao Makuu ya DCB Magomeni Mwembechai au kwa njia ya mtandao kupitia barua pepe shareholder@dcb.co.tz au matawini kabla ya saa nne asubuhi siku ya Ijumaa tarehe 18 Julai 2025.

3. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi (proxy forms) zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya benki (www.dcb.co.tz).

4. Orodha (Register) ya wanahisa itafungwa siku ya Jumanne tarehe 15 Julai, 2025.

5. Mapendekezo ya wanahisa yawasilishwe kwenye ofisi ya Katibu wa Benki au kwa barua pepe kabla ya saa nane kamili mchana siku ya Jumatano tarehe 16 Julai, 2025.

Kwa idhini ya Bodi,

**Bi. Regina Mduma**

Katibu wa Kampuni

26 Juni, 2025.

## 23.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 22 WA MWAKA

### KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 22 MWAKA ULIOFANYIKA TAREHE 14 SEPTEMBA 2024

Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa 22 wa mwaka wa benki ya DCB uliofanyika tarehe 14 September, 2024 kwa njia ya mtandao.

### WAJUMBE WA BODI WALIOHUDHURIA

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bi. Zawadia Nanyaro | Mwenyekiti wa Mkutano |
| 2. | Bw. Alexander Sanga | Mjumbe wa Bodi |
| 3. | Prof. emer Tadeo Satta | Mjumbe wa Bodi |
| 4. | Bw. David Shambwe | Mjumbe wa Bodi |
| 5. | Bi. Pamela Nchimbi | Mjumbe wa Bodi |
| 6. | Dkt. Amina Baamary | Mjumbe wa Bodi |
| 7. | Bw. Cliff Maregeli | Mjumbe wa Bodi |
| 8. | Bw. Onesmo Mwoga | Mjumbe Mbadala wa Bodi |
| 9. | Bw. Sabasaba Moshingi | Mkurugenzi Mtendaji |
| 10. | Bi. Regina Mduma | Katibu wa Benki |

### WAKURUGENZI WAANDAMIZI WA BENKI YA DCB

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Sabasaba Moshingi | Mkurugenzi Mtendaji |
| 2. | Bw. Leonard Katamba | Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji |
| 3. | Bi. Regina Mduma | Mkurugenzi wa Idara ya Sheria na Katibu wa Benki |
| 4. | Bw. Deogratius Thadei | Mkurugenzi wa Mikopo |
| 5. | Bi. Msingo Mkanzabi | Mkurugenzi wa Idara ya rasilimali watu |
| 6. | Bw. Ramadhan Mganga | Mkurugenzi wa Biashara |
| 7. | Bw. Emmanuel Barenga | Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani |
| 8. | Bw. Siriaki Kirki | Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Fedha |
| 9. | Bw. Emmanuel Mushi | Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti wa Viashiria Hatarishi |

### WAWAKILISHI KUTOKA KUNDI LA WANAHISA WAANZILISHI

| | | |
|---|---|---|
| 10. | Bw. Kateti Selemani | Halmashauri ya Jiji la Dar-es-Salaam na Manispaa ya Ilala |
| 11. | Bw. Onesmo Raphael Mwoga | Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni |
| 12. | Bw. Revocatus Mwita Mohabe | Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo |
| 13. | Bw. Faraja Makua | Halmashauri ya Manispaa ya Temeke |
| 14. | Bw. Frasto Kiwale | Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni |

### WAWAKILISHI KUTOKA KUNDI LA WANAHISA WA TAASISI

| | | |
|---|---|---|
| 15. | Bw. Medson Enock Chimande | UTT- Asset Management & Investor's Services Plc |
| 16. | Bw. Safi Julius | National Health Insurance Fund (NHIF) |

### WANAHISA BINAFSI

Orodha imeambatanishwa kama Kiambatanisho namba 1

### WAALIKWA

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Alex G. Mgongolwa | Mwanasheria Mshauri wa DCB |
| 2. | Bw. Baraka Palangyo | Wakaguzi Huru – Pricewaters Coopers |
| 3. | Bi. Mariam Omary | Mamlaka ya Masoko ya Mtaji na Dhamana (CMSA) |
| 4. | Bi. Jesca Jenge | Mamlaka ya Masoko ya Mtaji na Dhamana (CMSA) |
| 5. | Bi. Happynes Mushi | Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) |

### UTANGULIZI

Wanahisa walifahamishwa kwamba Mkurugenzi Mtendaji mpya wa benki, Bw, Sabasaba Moshingi aliripoti mnamo tarehe 1 Novemba 2024.

### AGENDA 1: KUTHIBITISHA AKIDI NA KUFUNGUA MKUTANO MKUU WA 22 WA MWAKA

Katibu wa Benki, kwa kushirikiana na Mwanasheria Mshauri wa Benki, walithibitisha kuwa kwa mujibu na Sheria ya Makampuni ya Tanzania pamoja na Katiba ya benki, Mkutano Mkuu ulihitaji akidi ya asilimia 75 ya wanahisa. Akidi ilithibitishwa kuwepo na hivyo Mkutano Mkuu ulifunguliwa rasmi saa nne na robo asubuhi.

### AGENDA 2: KURIDHIA AGENDA YA MKUTANO MKUU WA 22 WA MWAKA

Mwanasheria Mshauri wa benki alithibitisha kuwa taarifa ya Mkutano Mkuu wa 22 wa Mwaka ilitolewa kwa wakati kupitia magazeti, mitandao ya kijamii, tovuti ya benki, pamoja na ujumbe mfupi wa maandishi (SMS), uliotumwa kwa wanahisa wote. Mwanasheria Mshauri wa benki alieleza kwamba, kwa kuwa Katibu wa Kampuni hajapokea mapendekezo yeyote ya mabadiliko ya agenda, hivyo basi agenda ya Mkutano Mkuu wa 22 wa Mwaka iliyotangazwa ndio agenda ya kikao hicho.

***Wajumbe waliridhia agenda za Mkutano Mkuu wa 22 wa Mwaka.***

## AGENDA 3: KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 21 WA MWAKA

Wajumbe wa Mkutano Mkuu walipitishwa kwenye kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 21 wa Mwaka na waliridhia kumbukumbu hizo bila mapendekezo au maboresho yeyote.

## AGENDA 4: KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA 21 WA MWAKA

Wanahisa waliridhia rasmi utekelezaji wa maazimio na maagizo yote yaliyotolewa katika Mkutano Mkuu wa 21 wa Mwaka, na hivyo kutangaza kuwa yametekelezwa kikamilifu.

## AGENDA 5: TAARIFA YA WAKURUGENZI NA TAARIFA YA HESABU ZILIZOKAGULIWA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA, 2023

5.1 Wanahisa walipokea taarifa kutoka kwa Bodi ya Wakurugenzi ambayo imegawanyika kwenye makundi manne; barua ya Mwenyekiti wa Bodi, barua ya Mkurugenzi Mtendaji, taarifa za fedha za mwaka ulioishia 31 Disemba, 2023 na taarifa ya Mkaguzi Huru wa mahesabu kwa mwaka ulioishia 31 Disemba, 2023.

5.2 Iliripotiwa kwamba jumla ya wakurugenzi tisa (9) akiwamo Mkurugenzi Mtendaji walihudumia benki mwaka 2023 na hakuna Mkurugenzi aliyemiliki zaidi ya asilimia 5 ya jumla ya mtaji wa hisa wa benki.

5.3 Iliripotiwa kwamba kwa mwaka 2023 benki ilipata hasara baada ya kodi ya Tsh bilioni 3.6. Hasara hiyo ilitokana na ongezeko kubwa la gharama za riba kufuatia changamoto za ukwasi iliyoikumba sekta ya benki, upungufu wa fedha za kigeni, mfumuko wa bei za mafuta na ongezeko la tengo la mikopo chechefu. Bodi ya Wakurugenzi na menejimenti ya benki walifanya maamuzi ya kubadilisha mizania ya benki ili kuanza rasmi safari ya mageuzi itakayo badili historia ya DCB.

5.4 Iliripotiwa kwamba benki ilipata jumla ya mapato ya mwaka kabla ya tengo la mikopo chechefu la Tsh 12.7 bilioni, ikiwa imepungua kidogo ikilinganishwa na Tsh 15.2 bilioni zilizoripotiwa mwaka 2022. Jumla ya mali za benki ziliongezeka kutoka Tsh 211.9. bilioni (2022) hadi kufikia Tsh 230.9 bilioni (2023). Mikopo halisi ilikuwa Tsh 120.84 bilioni (2022), ikipungua kutokea Tsh 114.71 bilioni (2022). Hata hivyo, uwiano wa mikopo chechefu uliripotiwa kupungua kutoka 12.2% kwa mwaka 2022 hadi 6% mwaka 2023.

5.5 Iliripotiwa kwamba jumla ya gharama za uendeshaji zilikuwa kiasi cha Tsh 20.7 bilioni (2023) kutoka Tsh 20.6 bilioni (2022). Amana za wateja zilipungua kufika Tsh 140 bilioni kutoka Tsh141.9 bilioni mwaka 2022. Jumla ya thamani ya hisa ilipungua hadi kufikia Tsh 24.7 bilioni kutoka Tsh 28.4 bilioni mwaka 2022. Mapato halisi ya riba kwa mwaka 2023 yalikua Tsh 12.7 bilioni yakiwa yamepungua kutoka Tsh 15.2 mwaka 2022. Jumla ya mapato yasiyo ya riba yalipungua kutoka Tsh 10.2 mwaka 2022 kufika Tsh 6.4 bilioni mwaka 2023. Dhima za benki ziliongezeka kutoka Tsh 183.4 bilioni mwaka 2022 hadi kufikia Tsh 206.2 bilioni.

5.6 Iliripotiwa kwamba Bodi ya Wakurugenzi haikupendekeza malipo ya gawio kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2023 kwasababu benki haikukidhi vigezo vya uwiano wa gharama za uendeshaji na mapato ghafi wa asilimia 55 na mikopo chechefu wa asilimia 5, vilivyoainishwa na Benki Kuu ya Tanzania ili kupata malipo ya gawio.

5.7 Iliripotiwa kwamba katika mwaka 2023, mafanikio na maendeleo muhimu katika benki yalikuwa ni pamoja na kuingia katika makubaliano na kampuni ya Tigopesa ili kuruhusu wateja wa DCB kutumia mawakala wao kupata huduma za kuweka na kutoa pesa na kuzinduliwa kwa mfumo wa kidijitali wa uendeshaji wa VICOBA ili kuweka bayana na kuboresha utunzaji wa taarifa za vikundi. Pia mabadiliko yalifanyika katika nafasi muhimu za uongozi ili kufanikisha malengo ya benki; hii ikiwemo kumteua Mkurugenzi Mtendaji, Bwana Sabasaba Moshingi.

5.8 Iliripotiwa kwamba Bodi ya Wakurugenzi na menejimenti ya benki imeandaa mpango mkakati mpya wa miaka mitano kutoka 2024 hadi 2028 utakaohakikisha ukuaji endelevu wa benki. Mkakati huo umejikita katika mambo makuu matano: ukuaji wa mtaji wa angalau Tsh 10 bilioni kabla ya mwisho wa mwaka 2024 kupitia uuzaji wa hisa stahiki, ukuaji wa amana za wateja, uboreshaji wa mifumo ya kutolea huduma, ongezeko wa mikopo hadi Tsh bilioni 322 ifikapo mwaka 2028 huku tukidhibiti uwiano wa mikopo chechefu chini ya asilimia 4.5 na kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati. Kwa kuanza utekelezaji wa mpango mkakati, benki imeanzisha huduma maalumu kwa wanawake iitwayo Tausi na imeshahudumia zaidi ya wanawake 10,000 katika mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma.

5.9 Wakurugenzi walitoa shukrani za dhati kwa wadau wote waliowezesha mafanikio ya benki, wakiwemo wanahisa, wafanyakazi, wateja na mamlaka zote za uthibiti, kwa kuendelea kuiamini na kuiunga mkono benki ya DCB katika safari yake ya ukuaji na utoaji bora wa huduma za fedha.

5.10 Mkaguzi Huru wa Mahesabu kutoka PricewaterhouseCoopers (PwC) alieleza kuwa taarifa za fedha zilizokaguliwa ziliandaliwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu, kanuni za Benki Kuu ya Tanzania, na sheria nyingine husika. Mkaguzi huyo alithibitisha kwamba benki iko imara na hivyo akatoa hati safi ya ukaguzi.

Wanahisa walipokea taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi, walijadili na kutoa mapendekezo na kuuliza maswali kama ifuatavyo:

i. **Swali: Je, benki itafanya nini kuhakikisha kuwa wanahisa wanapata gawio na kwa wakati huo huo inabakisha mapato yatokanayo na faida ili kufanikisha mpango wa ukuaji wa benki, ikizingatia kuwa benki haijalipa gawio kwa muda mrefu.**

Jibu: Benki imejipanga kutafuta uwiano kati ya malengo ya muda mfupi na muda mrefu ya uwekezaji na kulipa gawio. Kama ilivyoelezewa awali, moja ya mkakati wa benki ni kupunguza mikopo chechefu na uwiano kati ya mapato na matumizi. Hata hivyo, pindi benki itakapopata faida ya kutosha, itaweka kipaumbele kwenye ulipaji wa gawio kwa wanahisa na kuhakikisha kwamba ukuaji wa benki hauathiriki.

ii. **Swali: Je Bodi imegundua nini kuhusu utendaji wa kitengo cha mikopo ambao umesababisha mikopo chechefu na hatimaye kuleta hasara kwa benki? Na je, ni mikakati gani ambayo benki imeweka ili kuhakikisha ufuatiliaji wa karibu na urejeshwaji wa mikopo iliyofutwa kwenye vitabu vya benki?**

Jibu: Benki imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya muundo wa idara ya mikopo ili kuongeza ufanisi, kuimarishwa kwa mfumo wa tathmini ya mikopo na utoaji wa taarifa kwa wakati kwa wateja na ufuatiliaji wa mikopo iliyochelewa au kufutwa.

iii. **Swali: Je benki ina timu yenye ufanisi wa kutosha kufanikisha mpango mkakati wake?**

Jibu: Benki ina timu imara yenye uwezo wa kuifikisha kutoka ilipo sasa hadi kufikia kwenye mafanikio yanayotarajiwa. Benki imefanya mabadiliko ya kiutendaji kwa kumuajiri Mkurugenzi Mkuu na Wakurugenzi Waandamizi wa idara zifuatazo: Tehama, Mikopo na Fedha. Wakurugenzi hawa wana uzoefu mkubwa wa biashara na kwa kushirikiana na wakurugenzi wengine watachangia kwa kiasi kikubwa kutekeleza mpango mkakati wa benki kwa ufanisi.

iv. **Swali: Je ni kwanini mapato yasiyo ya riba kati ya mwaka 2022 na 2023 yalipungua kutoka Tsh 4.2 bilioni hadi Tsh 1.2 bilioni? Je benki ina mikakati gani kuongeza mapato hayo muhimu?**

Jibu: Kwa mwaka 2022, benki ilifanya biashara kubwa kupitia mauzo ya hati fungani, ambapo iliingiza Tsh 3.1 bilioni. Hata hivyo, mwaka 2023 benki haikuwa na hati fungani za kuuza, hivyo haikuweza kupata mapato katika eneo hilo. Mpango Mkakati wa Benki wa mwaka 2024–2028, umelenga kuongeza mapato yasiyo ya riba ili kufikia kati ya asilimia 30 hadi 40 ya mapato yote ya benki. Hili ni eneo la kipaumbele na juhudi mbalimbali zinaendelea ili kufanikisha lengo hilo.

v. **Swali: Je benki ina mpango gani wa uwekezaji katika mtandao wa mawakala ili kuongeza upatikanaji wa huduma za fedha kwa wananchi.**

Jibu: Benki imekuwa ikiongeza mawakala wake mwaka hadi mwaka. Aidha, benki imeingia mkataba wa kimkakati na TigoPesa, utakaowawezesha wateja wa benki kutumia mawakala wa TigoPesa kama sehemu ya mtandao wa mawakala wa benki. Hii ni hatua muhimu katika kupanua wigo wa huduma na kuongeza ujumuishaji wa kifedha (financial inclusion), hasa katika maeneo ambayo hakuna matawi ya DCB.

vi. **Pendekezo:** Manispaa zimejielekeza katika mikakati ya kuongeza vyanzo vya mapato, hivyo benki inapaswa kuangalia namna ya kushirikiana na manispaa ili kufanikisha lengo hilo. Ingawa manispaa nyingi bado hazina uwezo wa kifedha wa kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo, zina uwezo wa kukusanya mapato kupitia miradi hiyo. Hivyo basi, benki iichukulie ili kama fursa ya kimkakati na kushirikiana na manispaa hizi kwa kutoa mikopo itakayosaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ushirikiano huo utawezesha manispaa kuongeza mapato na utoaji wa huduma kwa jamii, huku benki ikiongeza mtaji na kupanua wigo wa biashara zake.

vii. **Pendekezo:** Benki ijitahidi kuhakikisha mikutano ya wanahisa inafanyika mapema, ili taarifa ziwe na maana na mchango katika maamuzi ya wakati husika.

viii. **Pendekezo:** Benki inatakiwa kufanya marekebisho ya muundo wa Bodi ya Wakurugenzi, ambayo yatasaidia Bodi kusimamia utekelezaji wa Mipango Mkakati (2024-2028) wa benki.

ix. **Pongezi:** Wanahisa waliipongeza Bodi ya Wakurugenzi kwa kumteua Bw. Sabasaba Moshingi kama Mkurugenzi Mtendaji wa benki. Wanahisa walionesha kuwa na imani kubwa na uwezo wake huku wakirejea mafanikio aliyoyapata katika benki nyingine alizowahi kuongoza. Wanahisa walisema wanatarajia kuona mabadiliko chanya na maboresho katika utendaji wa benki kwa ujumla chini ya uongozi wake.

***Wanahisa walipokea na kuridhia Taarifa za Bodi ya Wakurugenzi na Hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2023.***

## AGENDA 6: KUPOKEA NA KUIDHINISHA PENDEKEZO LA KUONGEZA MTAJI WA BENKI KWA NJIA YA HISA STAHIKI

6.1 Iliripotiwa kwamba, kwa mujibu wa Kanuni za Utoshelevu wa Mitaji za Benki Kuu ya Tanzania za mwaka 2023 (Capital Adequacy Regulations, 2023), kila benki ya biashara inatakiwa kuwa na mtaji usiopungua Tsh bilioni 15 pamoja na uwiano wa mtaji wa angalau asilimia 12.5. Hali ya sasa ya mtaji wa benki ni hafifu na vilevile haiendani na mahitaji ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2024–2028).

6.2 Ilielezwa kuwa katika kikao chake cha tarehe 29 Februari 2024, Bodi ya Wakurugenzi iliidhinisha azimio la kuongeza mtaji wa benki kwa kiasi cha angalau Tsh bilioni 10 kupitia zoezi la uuzaji wa Hisa Stahiki. Kila mwanahisa atapewa haki ya kupata hisa moja ya ziada kwa kila hisa moja anayomiliki. Bodi ya Wakurugenzi iliomba idhini ya wanahisa kupitisha pendekezo la kuongeza mtaji wa benki wa angalau Tsh bilioni 10 kupitia Hisa Stahiki zitakazouzwa kwa bei ya Tsh 110 kwa kila hisa moja.

***Wanahisa waliridhia pendekezo la kuongeza mtaji wa benki kwa angalau Tsh bilioni 10 kupitia njia ya Hisa Stahiki, zitakazouzwa kwa bei ya Tsh 110 kwa kila hisa moja kwa wanahisa waliopo.***

## AGENDA 7: KUPOKEA TAARIFA YA KUISHA KWA MUDA, KUONGEZA MUDA NA UTEUZI WA WAJUMBE WA BODI

7.1 Bodi ya Wakurugenzi iliwasilisha ombi la kuongezewa muda wa uongozi wa wajumbe watatu wa Bodi, kwa kuzingatia Katiba ya benki, Sheria ya Benki Kuu kuhusu Utawala Bora, Muongozo wa Wakurugenzi uliotolewa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), pamoja na Sheria ya Makampuni.

7.2 Ilielezwa kuwa wajumbe watatu wa Bodi yaani, Dkt. Amina Baamary, Bw. Cliff Maregeli, na Bw. David Shambwe waliteuliwa na Mkutano Mkuu wa 19 wa Mwaka uliofanyika tarehe 12 Juni 2021, kwa kipindi cha miaka mitatu, ambacho sasa kimefikia ukomo. Mafanikio ya Wakurugenzi hao tangu walivyoteuliwa, ni pamoja na usimamizi thabiti wa benki na mageuzi ya kidijitali.

7.3 Bodi ya Wakurugenzi ilimtambulisha Bw. David Joshua Minja kama mjumbe mpya wa Bodi, anayewakilisha kundi la wanahisa binafsi. Bw. Minja ana uzoefu mkubwa katika biashara na masoko, akiwa ameihudumia sekta hiyo kwa zaidi ya miaka 20. Kwa kuzingatia ujuzi na thamani ya kimkakati anayoleta DCB, Bodi ilipendekeza uteuzi wake uidhinishwe rasmi na wanahisa.

Wanahisa walipokea taarifa za Bodi ya Wakurugenzi, walijadili kuuliza maswali na kutoa mapendekezo kama ifuatavyo:

i. **Swali: Je katiba ya benki inasema nini kuhusu kuongezwa muda kwa wajumbe wa Bodi? Je nafasi hizo zilitangazwa ili kuwapa watu wengine nafasi ya kuwania kwa ushindani?**

Jibu: Katiba ya benki, kupitia Kifungu cha 54(5), inatoa mamlaka kwa Bodi kupendekeza kuongezewa muda kwa mjumbe anayemaliza kipindi chake. Hakuna katazo la Bodi kufanya hivyo, ikiwa mjumbe huyo atatimiza masharti ya kuendelea. Kifungu cha 55(6a & 6b) kinaeleza kuwa mjumbe hataongezewa muda kama utendaji wake wa miaka mitatu iliyopita haukuridhisha ama alikiuka kanuni zinazompa sifa ya kuwa mjumbe wa Bodi.

ii. **Swali: Je wajumbe waliopendekezwa kwa kuongezewa muda wanawakilisha wanahisa wa kundi binafsi? Je wanachaguliwa na wanahisa wa kundi hilo pekee, au wanachaguliwa na wanahisa wote?**

Jibu: Dkt. Amina Baamary, Bw. Cliff Maregeli na Bw. David Minja ni wawakilishi wa kundi la wanahisa binafsi na Bw. David Shambwe ni mjumbe huru wa Bodi.

iii. Pendekezo: Katiba ya benki ifanyiwe marekebisho ili kuweka wazi taratibu zinazohusu, uwakilishi wa makundi mbalimbali ya wanahisa.

***Wanahisa waliridhia pendekezo la Bodi la kuongezwa muda kwa wajumbe watatu wa Bodi yaani, Dkt. Amina Baamary, Bw. Cliff Maregeli na Bw. David Shambwe kwa kipindi cha miaka mitatu. Aidha, Bw. David Minja aliteuliwa rasmi kuwakilisha kundi la wanahisa binafsi kwa kipindi cha miaka mitatu.***

## AGENDA 8: KUTEUA MKAGUZI HURU WA MAHESABU KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2024

Iliripotiwa kwamba Mkaguzi Huru wa Fedha kwa miaka sita iliyopita alikuwa PricewaterhouseCoopers (PwC). Sheria ya Benki Kuu inayosimamia wakaguzi huru wa nje hairuhusu Mkaguzi Huru kukagua benki kwa zaidi ya miaka sita mfululizo. Hivyo benki inalazimika kubadilisha Mkaguzi Huru wa Fedha. Mchakato wa uteuzi ulihusisha kampuni kubwa tatu za kimataifa ambazo ni KPMG Tanzania, Deloitte & Touche, na Ernst & Young. Bodi ilipendekeza KPMG Tanzania kuteuliwa kama Mkaguzi Huru wa Fedha kwa mwaka 2024 kwa gharama ya Tsh 140,989,527.

***Wajumbe waliridhia pendekezo la Bodi na kumteua rasmi KPMG Tanzania kama Mkaguzi Huru wa Fedha kwa mwaka wa fedha unaoishia 31 Disemba 2024 kwa Tsh. 140,989,527.***

## AGENDA 9: KUPOKEA NA KURIDHIA PENDEKEZO LA MALIPO YA ADA KWA WAJUMBE WA BODI

Wanahisa waliridhia pendekezo la Bodi la malipo ya ada kwa Wajumbe wa Bodi kuendelea kuwa Tsh 6,000,000 baada ya kodi kwa mwaka kwa kila Mjumbe wa Bodi.

## AGENDA 10: KUPANGA TAREHE YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA TATU

Wanahisa waliazimia kuwa Mkutano Mkuu wa 23 wa Mwaka ufanyike siku ya Jumamosi, tarehe 19 Julai 2025.

## AGENDA 11: MENGINEYO

Katibu wa Kampuni alithibitisha kwamba hakukuwa na agenda ya mengineyo iliyowasilishwa kabla ya Mkutano Mkuu.

Mkutano ulifungwa mnamo saa nane kamili mchana.

| | |
|---|---|
| **Zawadia Nanyaro**<br>**Mwenyekiti wa Bodi** | 19 Julai 2025<br>**Tarehe** |
| **Regina Mduma**<br>**Katibu wa Kampuni** | 19 Julai 2025<br>**Tarehe** |

## 23.4 KUPOKEA NA KURIDHIA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA MKUTANAO MKUU WA 22 WA MWAKA

| NA | AGIZO | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1 | Benki inapaswa kuangalia namna ya kushirikiana na manispaa kimkakati ili kufanikisha malengo ya benki na manispaa kwa upande mwingine. | Benki imetekeleza agizo hili kikamilifu na imekuwa ikishirikiana na manispaa za mkoa wa Dar es Salaam katika ukusunyaji wa mapato kupitia akaunti za kata (Ubungo, Jiji, Kinondoni na Temeke), kutoa mikopo ya asilimia kumi (Ubungo, Kinondoni na Temeke) na ukusanyaji wa kodi ya huduma (service levy).<br><br>Pia benki yetu imekuwa kinara katika shughuli mbalimbali za kijamii ikishirkiana na manispaa ikiwa ni pamoja na kuchangia na kushiriki upokeaji wa Mwenge katika manispaa za Dar es Salaam, kutoa madawati mashuleni na uzinduzi wa miradi mbalimbali. Aidha, benki imekua ikitoa elimu ya bure kwa wajasiliamali wadogo wadogo na wa kati. |
| 2 | Benki ijitahidi kuhakikisha Mkutano Mkuu wa Mwaka unafanyika mapema, ili taarifa zitumike kufanya maamuzi kwa wakati. | Benki imetekeleza agizo hili. Mwaka jana Mkutano Mkuu wa 22 wa Mwaka ulifanyika tarehe 14 Septemba 2025, mwaka huu Mkutano Mkuu wa 23 wa Mwaka umefanyika tarehe 19 Julai 2025 na benki inategemea kufanya Mkutano Mkuu wa 24 wa Mwaka tarehe 26 Juni 2026. |
| 3 | Benki ifanye marekebisho ya muundo wa Bodi ya Wakurugenzi. | Benki imetekeleza agizo hili na mapendekezo ya muundo mpya wa Bodi ya Wakurugenzi yameletwa kwenye Mkutano Mkuu wa 23 wa Mwaka. |
| 4 | Katiba ya benki ifanyiwe marekebisho ili kuweka wazi taratibu zinazohusu, uwakilishi wa makundi mbalimbali ya wanahisa. | Benki imetekeleza agizo hili na mapendekezo ya madiliko ya Katiba ya benki yameletwa kwenye Mkutano Mkuu wa 23 wa Mwaka. |

# 23.5 KUPOKEA TAARIFA YA WAKURUGENZI WA BODI

## 23.5.1 BARUA YA MWENYEKITI WA BODI KWA WANAHISA

KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2024



"Tuna imani kuwa usimamizi wetu wa pamoja utaanza kuleta matokeo chanya kwa wanahisa wetu."

Matokeo haya yanathibitisha dhamira yetu ya kuongeza thamani kwa wanahisa mwaka hadi mwaka. Thamani hisa ya DCB sokoni (market capitalization) iliongezeka hadi Tsh bilioni 22 kutoka Tsh bilioni 14.9 mwaka 2023, ikiashiria kuongezeka kwa imani ya wawekezaji na misingi imara ya biashara yetu. Dira yetu ya mageuzi inabaki kuwa thabiti, tukiwa na mipango ya kuongeza faida itokanayo na mtaji na kurejesha malipo ya gawio kwa wanahisa.

**Thamani hisa ya DCB sokoni (market capitalization) iliongezeka**

**47.65%**

**TSH BILIONI 22**

**TSH BILIONI 14.9: 2023**

**ikiashiria kuongezeka kwa imani ya wawekezaji na misingi imara ya biashara yetu.**



## Ndugu wanahisa,

**Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, nina furaha kuwasilisha kwenu Ripoti ya Mwaka na Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka wa fedha 2024.**

Kabla ya kuwasilisha ripoti hii, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati wanahisa wote kwa kuendelea kutuamini mliotupa majukumu ya kusimamia benki yetu na kushiriki kikamilifu katika zoezi la kuongeza mtaji wa benki kupitia uuzaji wa Hisa Stahiki (Rights Issue). Benki ilipata mtaji uliokusudiwa katika hatua mbalimbali kuanzia Novemba 2024 hadi Aprili 2025. Nawashukuru sana kwa ushiriki wenu. Nichukue nafasi hii kuwakaribisha rasmi wanahisa wote wapya waliowekeza katika benki ndani ya mwaka 2024 na 2025.

### Hali ya uchumi kwa mwaka 2024

Hali ya uchumi kwa mwaka 2024 iliambatana na changamoto na fursa mbalimbali. Uchumi wa taifa la Tanzania ulionyesha ustahimilivu, ambapo Pato la Taifa (GDP) liliongezeka kufikia asilimia 5.5 ikilinganishwa na asilimia 5.1 kwa mwaka 2023. Mfumuko wa bei uliendelea kuwa imara na thabiti kwa wastani wa asilimia 3 mwishoni mwa mwaka 2024, ikiwa ni ndani ya malengo yaliyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania. Soko la fedha za kigeni liliendelea kukua kutokana na uratibu mzuri wa sera pamoja na hali nzuri ya uchumi wa dunia. Sekta ya benki ilikumbwa na ukwasi na ukosefu wa fedha za kigeni.

Benki ya DCB ilikabiliana na changamoto za ndani na zilizoikumba sekta ya fedha nchini, ambazo ziliathiri matokeo yetu ya mwaka 2024. Changamoto hizo ni pamoja na uendeshaji wa benki kwa kutumia mtaji mdogo uliozuia ukuaji wa biashara, ukwasi na uhaba wa dola za kimarekani katika soko. Hali hii ilisababisha matokeo hafifu ya benki yetu, licha ya usimamizi imara katika utoaji wa mikopo na kupunguza gharama za uendeshaji.

### Utendaji wa benki kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba, 2024

Kwa mwaka 2024, benki inaripoti hasara baada ya kodi ya Tsh milioni 969, ikilinganishwa na hasara ya Tsh bilioni 3.6 kwa mwaka uliotangulia wa 2023. Hasara ya mwaka imepungua kwa asilimia 73% kutoka mwaka uliopita. Faida ya mtaji (ROE) ilikuwa -0.93% kwa mwaka 2024, ikilinganishwa na -22% mwaka 2023. Hii inaashiria matumizi bora ya mtaji na usimamizi makini wa fedha. Matokeo haya yanaonyesha kuwa mkakati wa benki wa miaka mitano umeanza kuzaa matunda na dhamira yetu ya kuongeza thamani kwa wanahisa mwaka hadi mwaka. Thamani ya hisa ya DCB sokoni (market capitalization) iliongezeka hadi kufikia Tsh bilioni 22 kutoka Tsh bilioni 14.9 mwaka 2023, ikiashiria kuongezeka kwa imani ya wawekezaji na misingi imara ya biashara yetu. Dira yetu ya mageuzi inabaki kuwa thabiti, tukiwa na mipango ya kuongeza faida itokanayo na mtaji na kurejesha malipo ya gawio kwa wanahisa.

### Pendekezo la gawio

Ingawa mwenendo wa utendaji wa benki unaendelea kuimarika, hatukuweza kupata faida ya kutosha kutoa gawio kwa mwaka wa fedha 2024. Bodi na Menejimenti wamejizatiti kuboresha utendaji kazi baada ya kuimarika kwa mtaji wa benki ili kurejesha thamani kwa wanahisa kupitia malipo ya gawio katika siku zijazo.




## Nafasi ya Bodi katika malengo ya kimkakati

Katika mwaka huu, Bodi ilisimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2024–2028) kwa kutoa mwelekeo sahihi, kutathmini utendaji wa menejimenti, na kuhakikisha matokeo yanalingana na dira ya benki. Bodi iliendelea kuwa makini katika kusimamia udhibiti wa viashiria hatarishi, kutoa mwelekeo katika mageuzi ya kidijitali, na kuimarisha mifumo ya utawala bora. Kamati zetu zilitimiza wajibu wake kwa usahihi ili kuhakikisha usimamizi wetu unatosheleza mahitaji ya uendeshaji katika mazingira magumu.

## Utawala bora

Mwaka 2024, benki iliendelea kuzingatia viwango vya juu vya utawala bora. Bodi ilipitia na kufanya marekebisho ya Katiba ya Kampuni (Memorandum and Articles of Association) ili kuendana na viwango vya utawala bora wa makampuni. Marekebisho haya yatawasilishwa katika mkutano huu kwa ajili ya maoni na kupitishwa kwa idhini ya wanahisa.

Muundo mpya wa umiliki wa wanahisa, unaleta madiliko kwenye wajumbe wa Bodi, wanaowakilisha kundi la wanahisa la taasisi baada ya uuzaji wa Hisa Stahiki. Tunaahidi kufanya kazi kwa karibu na wajumbe hawa wapya ili kuleta mageuzi chanya ya historia ya benki yetu.

## Mtazamo wa mbele

Matarajio ya uchumi wa Tanzania kwa mwaka 2025 ni ukuaji wa Pato la Taifa (GDP) hadi kufikia asilimia sita. Mkazo wetu utakuwa katika kulinda maslahi ya wanahisa kupitia usimamizi madhubuti na nidhamu ya fedha. Tutaendelea kuiunga mkono menejimenti katika kuongoza mageuzi ya kidijitali na kuongeza ufanisi wa kiutendaji kwenye maeneo yote ya biashara. Aidha, tutaongeza juhudi zetu katika ajenda ya ustawi wa jamii endelevu huku tukisimamia kwa makini mabadiliko yaletwayo na vihatarishi vipya, masuala ya mazingira, jamii na uongozi bora ili kuendelea kutumia fursa zinazojitokeza kwa ufanisi zaidi.

## Shukrani

Shukurani za pekee ziwafikie wanahisa wetu kwa imani mlilonayo katika benki ya DCB na ushirikiano wenu katika kipindi hiki cha mabadiliko. Pia nawashukuru wajumbe wenzangu wa Bodi na wafanyakazi wa DCB kwa juhudi zenu, uaminifu na ustahimilivu katika utekelezaji wa majukumu yenu. Shukurani za pekee ziwafikie mamlaka mbalimbali zinazotusimamia ikiwa ni pamoja na: Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na mamlaka zote za udhibiti kwa miongozo na msaada mbalimbali.

Mwisho, naomba niwashukuru wateja wetu wote – asanteni kwa kuichagua benki ya DCB kuwa mshirika wenu wa kifedha; imani yenu ndiyo rasilimali yetu kubwa zaidi. Tunaamini kuwa mikakati tunayoitekeleza sasa, pamoja na usimamizi makini wa ufanisi, uthibiti wa viashiria hatarishi, na kutumia fursa mbalimbali zinazopatikana katika sekta ya fedha jumuishi, zitaifanya benki kuwa na msingi imara zaidi, faida endelevu na mustakabali bora. Tunatarajia kushiriki nanyi mafanikio yetu katika vipindi vijavyo.

**Zawadia Nanyaro**
Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi
DCB Commercial Bank PLC

# CHAIRPERSON'S LETTER TO SHAREHOLDERS
FOR THE FINANCIAL YEAR ENDED 31 DECEMBER 2024



"Our efforts in robust risk management to maintain a healthy asset portfolio."

These results affirm our commitment to increasing our shareholders' value year on year. Our market capitalisation increased to TZS 22 billion from TZS 12.69 billion in 2023. This performance underscores growing investor confidence and the strong fundamentals of our business.

**Our market capitalisation increased to**

**47.65%**

**TZS 22 BILLION**

**TZS 12.69 BILLION: 2023**

**This performance underscores growing investor confidence and the strong fundamentals of our business.**



## Dear esteemed shareholders,

**On behalf of the Board of Directors, it is my privilege to present to you the Annual Report and Audited Financial Statements for DCB Commercial Bank PLC for the financial year ended 31 December 2024.**

Before I present these reports, I would like to take this opportunity to sincerely thank the shareholders for believing in us and in our bank and thus participating in the capital increase exercise, through the rights issue. The bank was able to receive the full targeted capital in different stages from November 2024 to April 2025. I thank you all for your participation and welcome on board new strategic shareholders in the bank.

### Macroeconomic

The year 2024 economic environment presented both challenges and opportunities. The national economy demonstrated commendable resilience, with Gross Domestic Product (GDP) growth at 5.5% from 5.1% in 2023. Inflation remained low and stable, averaging 3%, well within the Bank of Tanzania's target, while the foreign exchange market saw improvements due to favourable global conditions and enhanced policy coordination. The external sector also showed significant improvement, and the public debt remained sustainable. The banking sector, including DCB Commercial Bank, faced increased pressures from tighter liquidity conditions and heightened credit risks, reflecting broader global economic uncertainties. These factors contributed to the subdue financial performance, as we prudently managed our loan portfolio and operational costs in a cautious macroeconomic climate.

However, despite this enabling environment, DCB Commercial Bank PLC faced specific internal and market-driven challenges that contributed to our financial outcome. Our performance was impacted with the operations with the low capital level which could not sustain the business expansion, low liquidity ratio, scarcity of US Dollars in the market, impacting the bank's non-funded income and tightened liquidity.

### Bank's performance for the financial year ended 31 December 2024

This year, we report a net loss of TZS 969 million, following a loss of TZS 3.6 billion in the preceding year, 2023. These results show that our strategy has started to yield results and has reduced our loss by 73% from the previous year. Our Return on Equity (ROE) of -0.93% in 2024 has improved from that of -22% in 2023, reflecting enhanced capital efficiency and prudent financial stewardship. These results affirm our commitment to increasing our shareholders' value year on year. Our market capitalisation increased to TZS 22 billion from TZS 12.69 billion in 2023. This performance underscores growing investor confidence and the strong fundamentals of our business. DCB's vision for turnaround remains bold with plans to increase our return on equity and resume dividend payment consistently.




## Dividend payout

Although the bank's performance trajectory is improving, the bank did not get a profit to enable it to pay a dividend for the financial year ending 31 December 2024. The Board and Management is committed to improve its performance after improved capital position through rights issue and return the shareholder's value through dividend payment in the near future.

## Role of the Board on strategic objectives

During the year, the Board provided active oversight of the five years strategic plan (2024 – 2028) by providing clear direction, evaluating performance of the executive management and ensure proper alignment with the bank's vision. The Board and Management have undertaken a rigorous review of our operations and strategic direction. We are implementing decisive measures to return the Bank to profitability and ensure sustainable growth. We remained vigilant in overseeing risk, supporting digital transformation, and strengthening our governance frameworks. Our committees worked diligently to ensure that our oversight remained fit for purpose in difficult operating environment where the bank spent 11 months below the regulatory capital margins.

## Corporate governance

In 2024, DCB Commercial Bank PLC continued to practice high standards of corporate governance in its operations, ensuring strong risk management and financial stability. The Board reviewed its Memorandums and Articles of Association as advised by the shareholders and to align with the best practice in Corporate Governance. These changes will be presented in this meeting for your deliberation and approval.

The Board expects changes in its composition resulting from shifts in the shareholding structure, particularly within the institutional shareholders' category, following the sale of rights shares. We look forward to working closely with the new Board members to drive transformative changes that will shape the future of our bank. We are confident that our joint oversight will begin to yield positive outcomes for our shareholders and all stakeholders.

Beyond these core pillars in governance, we are redoubling our efforts in robust risk management to maintain a healthy asset portfolio and fostering a culture of innovation and performance across all levels of the Bank.

## Outlook

The future outlook of Tanzanian's economy in 2025 expects the GDP to rise to 6%, the key drivers being investment in infrastructure, particularly in transport and logistics and stable power supply. Our focus will centre on safeguarding the interests of our shareholders through strong oversight and disciplined financial management. We will keep supporting the management as they lead in driving digital innovation and enhancing operational efficiency across all areas of the business. At the same time, we are deepening our commitment to drive the sustainability agenda by incorporating climate risk management and observing the best practices.

## Appreciation

I extend my sincere gratitude to our valued shareholders for your continued patience, trust, and unwavering support during this challenging transition period. To our dedicated employees and management team, your hard work, commitment, and resilience are the backbone of our operations, and we appreciate your tireless efforts. We are also grateful to the Bank of Tanzania, Capital Market and Securities Authority and other regulatory bodies for their guidance and support. Finally, to our loyal customers, thank you for choosing DCB Commercial Bank PLC as your financial partner; your trust is our greatest asset.

We are confident that the strategic initiatives we are undertaking, coupled with a vigilant focus on efficiency, risk management, and leveraging the immense opportunities in Tanzania's digital and inclusive finance sectors, will pave the way for a stronger, more profitable, and sustainable future for the bank. We look forward to sharing our progress with you in the coming periods.

Sincerely,

Zawadia Nanyaro
Chairperson of the Board of Directors
**DCB Commercial Bank PLC**

# 23.5 KUPOKEA TAARIFA YA WAKURUGENZI WA BODI

## 23.5.2 UJUMBE WA MKURUGENZI MTENDAJI KWA WANAHISA
KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2024



"Mizania yetu ya fedha ilibaki imara, ambapo jumla ya mali za benki ziliongezeka hadi kufikia kiasi cha Tsh bilioni 259.1."

"Mapato yatokanayo na riba yaliongezeka na kufikia Tsh bilioni 32.28"

"Benki ilipunguza hasara kutoka Tsh bilioni 3.6 iliyorekodiwa mwaka 2023 hadi kufikia Tsh milioni 969, mwaka 2024."



**73%**
**Hasara imepungua**

**16%**
**Mapato yatokanayo na riba**

12%
**Ongezeko la Mizania**

## Ndugu wanahisa,

**Kwa mwaka wa Fedha 2024, benki yetu ilipitia kipindi cha mabadiliko muhimu ambapo tulianza kuweka misingi imara ya kuirudisha benki kwenye kupata na faida endelevu. Licha ya changamoto na mabadiliko ya uchumi ndani na nje ya nchi, benki yetu ilijikita katika kuongeza mtaji ili kuboresha uendeshaji wake, kuongeza ufanisi kwenye utendaji, na kujiandaa kukua kama ilivyoainishwa kwenye Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2024 – 2028).**

Tunaamini kwa dhati kuwa mafanikio ya kweli katika miaka ijayo yatapatikana kwa kuimarisha misingi thabiti, hii inajumuisha kuimarisha mtaji wa benki, kuboresha utawala bora na kuwekeza kwenye teknolojia. Hatua tulizochukua ni muhimu sana katika kujenga taasisi imara inayoweza kuhimili changamoto za maendeleo endelevu. Hatua hizi zimeanza kuzaa matunda na matokeo ya mwaka 2024 yanadhihirisha kwamba mpango mkakati wetu uko imara na benki itaanza kupata faida hivi karibuni.

### Ufanisi katika mazingira magumu

Mwaka 2024, benki ya DCB ilipiga hatua muhimu katika safari yake ya mageuzi, ambapo imeonekana dhahiri kwamba Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2024-2028) umeanza kuzaa matunda. Benki ilipunguza hasara kutoka Tsh bilioni 3.6 iliyorekodiwa mwaka 2023 hadi kufikia Tsh milioni 969, mwaka 2024. Mafanikio haya yanaonyesha dhamira yetu ya kuirudisha benki katika kupata faida endelevu.

Mapato yatokanayo na riba yaliongezeka kwa asilimia 16 kufikia Tsh bilioni 32.28. Ongezeko hili lilichangiwa na ukuaji wa kitabu cha mikopo kwa kiasi cha Tsh bilioni 24.87. Mkakati wetu wa kukuza mikopo bora na safi, hasa mikopo midogo midogo (microfinance), umeonyesha mafanikio makubwa baada ya kuzindua bidhaa mpya ya mikopo ya vikundi vya wanawake, maarufu kama Tausi. Mafanikio haya yamethibitisha dhamira yetu ya kukuza ujumuishaji wa kifedha na maendeleo ya jamii.

Hata hivyo, gharama zitokanazo na riba ziliongezeka kwa asilimia 27 hadi kufikia kiasi cha Tsh bilioni 19.23 (kutoka Tsh bilioni 15.09 mwaka 2023); hii ilitokana na mazingira magumu ya ukwasi na gharama ya zoezi la kuongeza mtaji, japokuwa hali hii ni ya mpito. Tunaendelea kuchukua hatua thabiti ili kuboresha muundo wa vyanzo vya fedha na kupunguza gharama zake ikiwa ni pamoja na kuongeza juhudi za uhamasishaji wa amana nafuu na kuboresha mikakati yetu ya ukusanyaji wa madeni.

Mizania yetu ya fedha ilibaki imara, ambapo jumla ya mali za benki ziliongezeka kwa asilimia 12.2 hadi kufikia kiasi cha Tsh bilioni 259.1. Hii ilichangizwa na ukuaji wa mikopo na uwekezaji katika hatifungani za serikali. Amana za wateja ziliongezeka kwa asilimia 8.6 hadi kufikia Tsh bilioni 152. Mtaji wa benki uliongezeka kwa kiasi kikubwa baada ya mafanikio katika zoezi la uuzaji wa Hisa Stahiki (Rights Issue), ambapo uwiano wa mtaji wa daraja la kwanza ulifika asilimia 15.68 na daraja la pili ulifika asilimia 16.03. Benki ilifanya madiliko makubwa ya kiutendaji ambayo yalipunguza



Kufuatia Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2024–2028), ninafuraha kuwafahamisha **mafanikio yaliyopatikana katika nguzo muhimu za Mpango Mkakati wetu.**

uwiano wa gharama na mapato kupungua kutoka asilimia 108 mwaka 2023, hadi kufikia asilimia 97.98 mwana 2024. Pia faida kwa hisa (ROE) iliimarika hadi kufikia asilimia -0.93 mwaka 2024 kutoka -22% mwaka 2023. Hii yote ikiashiria msingi wa mafanikio ya muda mrefu.

### Maendeleo kwenye vipaumbele mkakati

Kufuatia Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2024–2028), ninafuraha kuwafahamisha mafanikio yaliyopatikana katika nguzo muhimu za Mpango Mkakati wetu. Katika eneo la mtaji, benki ilifanikiwa kutekeleza azimio la kuongeza mtaji kupitia uuzaji wa Hisa Stahiki, ambapo lengo la kuongeza mtaji kwa angalau Tsh bilioni 10 lilifanikiwa. Zoezi hili lilivutia wawekezaji wapya wa kimkakati (strategic partners), ambao wamejiunga na benki na hivyo kuimarisha ukwasi na kuongeza uwezo wa benki katika kupata amana za bei nafuu.

Kwa kuzingatia mkakati wetu wa ujumuishi wa kifedha (financial inclusion) na ukuaji wa kitabu cha mikopo, benki ilianzisha bidhaa ya mikopo inayotolewa kwa wanawake tuu. Bidhaa hii imekuwa bora na imara, na kufanya vizuri ikilinganishwa na bidhaa nyingine zote katika benki kwa mwaka 2024. Mikopo kwa wateja iliongezeka kwa asilimia 9.97%, hasa kutoka katika sekta za biashara ndogo ndogo na za kati (MSME/SMEs). Aidha, benki imeimarisha misingi ya utoaji wa mikopo ya kidijitali ili kuweza kuwafikia wateja wetu popote walipo nchini.

Pia, benki ilipiga hatua katika ukusanyaji wa amana kwa asilimia 8.56, hii ilitokana na mahusiano mazuri tuliyotengeneza na taasisi mbalimbali za kifedha. Ili kuweza kufanikisha shughuli za kiutendaji, Bodi na Menejimenti ya benki ilifanya mabadiliko ya kiutendaji ambayo yameleta matokea chanya katika uwajibikaji na kuboresha utoaji wa huduma katika maeneo mbalimbali.

Ingawa bado kuna kazi kubwa mbele yetu, tunatambua kwamba mafanikio yetu yanaenda hatua kwa hatua, na mwaka 2024 tumethibitisha kwamba mpango mkakati wetu unaenda sambasamba na dira yetu ya kuwa taasisi ya kifedha inayoaminiwa kwa kutoa huduma bora nchini.

### Mtazamo kwa mwaka wa fedha 2025 na zaidi.

